


Mchungaji Tony Alamo | Taifa la Kikristo la Alamo | Toleo 18700



*Mchungaji Tony na Susan Alamo, Okestra, na kwaya katika kipindi chao cha kimataifa cha televisheni. Picha ilichukuliwa mnamo mwaka 1974.*

# JE! MUNGU ANAMPA MWANAMKE HAKI YA KUTOA MIMBA IWAPO NI MHANGA WA UBAKAJI?

**na Tony Alamo**

MUNGU anasema, "Tazama, roho zote ni mali YANGU; kama vile roho ya baba ni mali YANGU, ndivyo ilivyo roho ya mwana. Mali YANGU; roho itendayo dhambi, itakufa. Bali kama mtu ni mwenye haki, na kuyatenda yaliyo halali na haki; hakula juu ya milima [kuabudu sanamu], wala hakuviinulia macho vinyago vya nyumba ya Israeli, wala hakumtia unajisi mke wa jirani yake [kuzini naye], wala hakumkaribia mwanamke wakati wa kutengwa kwake; wala hakumdhulumu mtu, bali amemrudishia mdeni wake rehani yake, wala hakumnyang'anya mtu mali yake kwa nguvu, naye amewapa wenye njaa chakula chake, na kuwavika nguo walio uchi; ambaye hakumkopesha mtu ili apate faida, wala hakupokea ziada ya namna yoyote; naye ameuepusha mkono wake na uovu, na kufanya hukumu ya haki kati ya mtu na mwenzake; tena ikiwa amezifuata sheria ZANGU, na kuzishika hukumu ZANGU; mtu huyu ni mwenye haki; hakika ataishi, asema BWANA MUNGU.

"Walakini akizaa mwana aliye mnyang'anyi, mmwaga damu, atendaye mambo hayo mojawapo; wala hakutenda mojawapo la mambo hayo yampasayo, bali amekula juu ya milima [kuabudu sanamu], na kumtia unajisi mke wa jirani yake [kuzini naye], na kuwadhulumu maskini na wahitaji, na kuwanyang'anya watu mali yao kwa nguvu, wala hakurudisha rehani [hajalipa zaka zao], naye ameviinulia macho vinyago, na kufanya machukizo, naye amekopesha watu ili apate faida na kupokea ziada; Je! Ataishi [milele] baada ya hayo? La, hataishi [milele]; amefanya machukizo hayo yote; hakika atakufa; damu yake itakuwa juu yake.

"Na kama yeye huyo akizaa mwana, naye ameona dhambi zote za baba yake alizozitenda, akaogopa, asifanye neno lolote kama hayo; hakula juu ya milima [kuabudu sanamu], wala hakuviinulia macho vinyago vya nyumba ya Israeli, wala hakumtia unajisi mke wa jirani yake [kuzini naye], wala hakumdhulumu mtu, wala hakutwaa kitu kiwekwe rehani [hakuzuia zaka na sadaka zake], wala hakumnyang'anya mtu mali yake kwa nguvu, bali amewapa wenye njaa chakula chake, na kuwafunika nguo walio uchi; tena ikiwa ameuzuia mkono wake asimwonee maskini, wala hakupokea faida na ziada, naye amezifanya hukumu ZANGU, na kuzifuata sheria ZANGU; hatakufa huyu kwa sababu ya uovu wa baba yake, hakika ataishi [milele]. Kwa habari za yule baba yake, kwa sababu aliwaonea watu kwa ukali mwingi, na kumnyang'anya ndugu yake mali yake kwa nguvu; na kuyatenda yasiyo mema kati ya watu wake, tazama, atakufa [milele] katika uovu wake.

"Lakini ninyi mwasema, kwani yule mwana asiuchukue uovu wa baba yake? Yule mwana atakapofanya yaliyo halali na haki, na kuzishika mari ZANGU na kuzitenda, hakika ataishi [milele]. Roho itendayo dhambi,

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

# JE! MUNGU ANAMPA MWANAMKE HAKI YA KUTOA MIMBA IWAPO NI MHANGA WA UBAKAJI?

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)*

ndiyo itakayokufa [milele]; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki ya mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake.

"Lakini mtu mbaya akighairi; na kuacha dhambi zake zote alizozitenda, na kuzishika amri ZANGU zote, na kutenda yaliyo halali na haki, hakika ataishi [milele], hatakufa [milele]. Dhambi zake zote alizozitenda hazitakumbukwa juu yake hata mojawapo; katika haki yake aliyoitenda ataishi. Je! Mimi ninafurahia kufa [milele] kwake mtu mwovu? Asema BWANA MUNGU; si afadhali kwamba aghairi, na kuiacha njia yake, akaishi [milele]?" (Ezekieli 18:4-23).

MUNGU hasemi tu kuwa roho zote ni ZAKE, lakini katika Hesabu 16:22, Musa na Haruni walisema YEYE ni "MUNGU wa roho za wenye mwili WOTE." Katika Yeremia 32:27 MUNGU anasema, "Mimi ni BWANA, MUNGU wa WOTE wenye mwili." MUNGU, katika Yeremia 1:5, alimwambia, "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua."

Jinsi gani mtu yeyote aweza kuwa na ujasiri wa kuiharibu nafsi, roho na mwili wa mtoto yeyote mchanga wa mwanadamu ambaye MUNGU alimjua kabla kuumbwa katika tumbo, waache kabla ya kutoka tumboni, hata katika tukio la kubakwa?

Sheria halisi ni sheria ya MUNGU.[1] Hebu tuone sheria ya MUNGU inavyosema: "Akifumaniwa mtu mume amelala na mwanamke aliyeolewa na mume, na wafe [kimwili na kiroho] wote wawili, mtu mume aliyelala na mwanamke, na yule mwanamke naye; ndivyo utakavyoondoa uovu katika Israeli. Pakiwa na kijana aliye mwanamwali ameposwa na mume [amechumbiwa], na mwanamume akimkuta mjini, akalala naye; watoeni nje katika lango la mji ule, mkawapige kwa mawe hata wafe; yule kijana, kwa kuwa hakupiga kelele, naye yu ndani ya mji; na yule mume, kwa kuwa amemtweza mke wa mwenzake; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako. Lakini yule mtu mume kama akimkuta kondeni kijana aliyeposwa, naye mume akamtenza nguvu [akambaka], akalala naye; yule mtu mume aliyelala naye na afe pekee; lakini yule kijana usimfanye neno; hana dhambi yule kijana ipasayo kuuawa: kwa kuwa ni mfano wa mtu kumwondokea mwenzake akamwua, ni vivyo lilivyo jambo hili: kwani alimkuta kondeni, yule kijana aliyeposwa akalia [akalia kuomba msaada kwa sababu hakutaka kubakwa], pasiwe na mtu wa kumwokoa [ili asibakwe]. Mtu mume akimwona kijana aliye mwanamwali ambaye hajaposwa, akamshika na kulala naye [akambaka], wakaonekana; yule mtu mume aliyelala naye na ampe baba yake yule kijana shekeli hamsini za fedha, kisha na awe mkewe, kwa kuwa amemtweza; hana ruhusa ya kumwacha [kumpa talaka] siku zake zote" (Kumbumkumbu la Torati 22:22-29).

Kwa mara ya kwanza nilipoiona sheria hii nilifikiria, "Mwanamke awezaje kutaka kuolewa na mwanaume yeyote ambaye alimbaka?" Kisha kwa haraka, akili yangu ilirudi nyuma hadi miaka arobaini na nane iliyopita katika ofisi ya mwanasheria katika Beverly Hills ambapo kwa mara ya kwanza nilifahamiana na MUNGU. ALINIAMURU kuwaambia watu katika ofisi ile kwamba YESU KRISTO ALIKUWA ANAKUJA duniani tena. ROHO WA MUNGU alikuwa juu yangu kwa nguvu ya namna hiyo, nami nilianza kuhojiana NAYE, nikisema, "BWANA, nitawaambia kesho. Nitawapigia simu. Nitawatumia nyaya, telegramu, lakini usinifanye niwaambie sasa." Ofisi ilikuwa imejazwa na wasaidizi wa watu wangu na watu wengine kutoka tasnia ya filamu. Nilidhani wangenikamata na kunipeleka kwenye hifadhi ya wendawazimu kama ningefanya kile ALICHOKUWA AKINIAMBIA kusema na kufanya. Hivyo MUNGU ALIANZA kuivuta roho yangu, nafsi yangu, ndani na nje ya mwili wangu, na kunifahamisha kuwa kama nisingesema kile ALICHONIAMBIA kusema, ningekufa saa ile papo hapo. Hapakuwa na chochote ambacho ningeweza kufanya KUMZUIA kuniua. Wakati huo huo, nilikuwa nikihisi jinsi ALIVYOKUWA na nguvu na akili nyingi, na nilifahamu kuwa hakuna yeyote aliyeweza KUMZUIA kufanya lolote ALILOTAKA kulifanya. Kabla ya jambo hili kunitokea, sikuwahi kumwamini MUNGU au YESU. Nilifahamika kama wakala bora wa matangazo katika aina yoyote ya biashara ikiwa ni pamoja na biashara za maonyesho. Tokea siku ile na kuendelea, niliacha kuwa wakala wa matangazo na nikaanza kumtafuta BWANA. Sina tatizo kuamini chochote alichosema MUNGU au asemacho. Kama MUNGU anamwambia mwanamume ni lazima amuoe mwanamke aliyembaka ambaye hajaolewa na kuishi naye maisha yake yote, na kisha anamwambia mwanamke kuwa lazima aolewe na mwanamume huyo na awe tayari kuishi naye hadi atakapokufa, ningependekeza kuwa wafanye hasa kile MUNGU anachowaamuru kufanya.

Tena, mara ya kwanza nilipoiona sheria hii, ilionekana kuwa kali kwangu. Sasa kwa kuwa namjua MUNGU na nguvu zake YAKE, najua pia kwamba YEYE ni BOSI. Unajua, wanawake wa leo wanabaka kirahisi. Wanaweza kuonekana kama malaika, lakini sivyo walivyo. Nimekutana na




HUDUMA ZA ALAMO MTANDAONI
www.alamoministries.com


**1** Kut. 20:3-17, Zab. 111:7-8, 119:89, 152, 160, Mit. 3:1-2, Isa. 40:8, Yer. 23:29, Dan. 7:9-10, Mal. 4:4, Mat. 5:17-19, Mk. 13:31, Rum. 3:31, Yak. 2:8-13, 1 Pet. 1:23-25, Ufu. 20:12-13

wengi wao ambao wanaonekana kama malaika lakini nimegundua ni waongo na ibilisi.

Mwanamke akiwa na mimba kwa sababu alibakwa, asiitoe. Akiitoa, huo utakuwa uuaji nambari moja, na atakwenda Jehannamu kwa sababu hiyo. Kutoka 20:13, Kiebrania cha awali, kinasema, "Usiue," na yeyote atakayeua ni lazima auawe. "Uuaji" ni pamoja na wa watoto wachanga wasiozaliwa. "Mtu awaye yote ampigaye mtu, hata akafa, hana budi atauawa huyo" (Kutoka 21:12). Nini kitatokea kwa wauaji wote? "Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na WAUAJI, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili" (Ufunuo 21:8). Na watu ni waongo kwa kusema kuwa watoto ambao hawajazaliwa si watu na si hai. Kama watoto hawa wachanga si hai, basi wanawezaje kuwaua? Na kwa nini wawaue kama si hai?

Wale wanaotoa mimba na wale wanaofanya kazi ya kutoa mimba, na wale walipua mabomu ya kujiua wote ni WAUAJI. Unapaswa kutubu sasa kwa sababu hukumu inakuja upesi kuliko unavyofikiri.

Katika Kutoka 21:22-25, tunaona adhabu ya kutoa mimba kwa bahati mbaya. "Watu waume wakiteta pamoja, wakamwumiza mwanamke mwenye mimba hata akaharibu mimba, tena yasiwe madhara zaidi; sharti atatozwa mali kama atakavyomwandikia mume wa huyo mwanamke; atalipa kama hao waamuzi watakavyosema. Lakini kwamba pana madhara zaidi, ndipo utatoza UHAI KWA UHAI, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu, kuteketeza kwa kuteketeza, jeraha kwa jeraha, chubuko kwa ajili ya chubuko." Mtoto anayekua tumboni mwa mama ni hai.

Katika Mathayo 22:31b-32, YESU alisema, "Hamjalisoma neno lililonenwa na MUNGU, akisema, Mimi ni MUNGU wa Ibrahimu, na MUNGU wa Isaka, na MUNGU wa Yakobo? MUNGU si MUNGU wa wafu bali wa walio HAI." Tena, mtoto anayekua tumboni mwa mama yu HAI na anakua, na MUNGU ni baba wa mtoto wa mwanadamu.[2]

Waabudu sanamu wanajulikana vyema kwa uuaji wa watoto wao wenyewe, hadi siku hii ya leo. Yeremia 32:35 inasema, "Tena walijenga mahali palipoinuka kwa Baali, palipo katika bonde la mwana wa Hinomu, ili kuwapitisha wana wao na binti zao katika moto [mauaji/kuavya mimba] kwa ajili ya Moleki, jambo nisilowaagiza; wala HALIKUNIINGIA moyoni MWANGU kwamba walitende chukizo hilo; wapate kumkosesha Yuda."

Makahaba wawili walimjia mfalme Sulemani, mtu mwenye hekima kuliko wote duniani,[3] wakiwa na mgogoro: "Ndipo wanawake wawili, makahaba, walimwendea mfalme, wakasimama mbele yake. Na mwanamke mmoja akasema, Ee bwana wangu, mimi na mwanamke huyu tunakaa katika nyumba moja; nami nalizaa nilipokuwa pamoja naye nyumbani. Kisha, siku ya tatu baada ya kuzaa kwangu, ikawa mwanamke huyu naye akazaa; na sisi tulikuwa pamoja; hapakuwa na mtu mwingine pamoja nasi nyumbani, isipokuwa sisi wawili tu.

"Na mtoto wa mwanamke huyu akafa usiku, maana alimlalia. Akaondoka kati ya usiku, akamwondoa mtoto wangu ubavuni pangu, mimi mjakazi wako nilipokuwa usingizini, akamweka kifuani pake, na mtoto wake mwenyewe, aliyekuwa amekufa, akamweka kifuani pangu, nilipoondoka asubuhi nimnyonyeshe mtoto wangu, kumbe? Amekufa. Hata asubuhi nilipotazama sana, kumbe! Siye mtoto wangu niliyemzaa. Ndipo yule mwanamke wa pili akasema, Sivyo hivyo; bali mtoto wangu ndiye aliye hai, na mtoto wako ndiye aliyekufa. Na mwenzake akasema, Sivyo hivyo; bali mtoto wako ndiye aliyekufa, na mtoto wangu ndiye aliye hai. Ndivyo walivyosema mbele ya mfalme. Ndipo mfalme akasema, Huyu anasema, Mtoto wangu yu hai, na mtoto wako amekufa. Na huyu anasema Sivyo hivyo; bali mtoto aliyekufa ni wako, na mtoto aliye hai ni wangu. Mfalme akasema, nileteeni upanga. Wakaleta upanga mbele ya mfalme. Mfalme akasema, mkate mtoto aliye hai vipande viwili, kampe huyu nusu na huyu nusu.

"Ndipo mwanamke yule, ambaye mtoto aliye hai ni wake, akamwambia mfalme kwa maana moyoni mwake alimwonea mtoto wake huruma, akasema, Ee bwana wangu, mpe huyu mtoto aliye hai, wala usimwue kamwe. Lakini yule mwingine akasema,

*(Inaendelea ukurasa wa 4)*

2 Amu. 13:5, Ayu. 31:15, Isa. 49:5, Yer. 1:5, Lk. 1:15, 39-41

3 1 Fal. 4:29-34, 2 Nya. 1:7-12

## Chile

*(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)*

Mpendwa Mchungaji Tony,

Salamu katika pendo la Bwana Yesu. Tunatumaini na tunajua kwamba majeshi ya malaika wake yanakulinda na kukutunza, na usisahau kwamba hauko peke yako. Unaye Mungu, malaika zake na watoto wa Mungu wanaokusaidia kwa kila jambo.

Ndugu, nalihitaji sanduku kubwa la maandiko yaliyogawanywa, majarida na Biblia mbili kubwa na Biblia tano za kawaida. Nyaraka zako zote zinasambazwa zikiwa zimepakwa mafuta na Mungu na zimekuwa Baraka kwa wale wanaozipokea. Kazi yako haitakuwa bure kamwe. Mungu atakulipa, kuwa na uhakika wa jambo hilo.

Jose Barria — Región de los Lagos, Chile

# JE! MUNGU ANAMPA MWANAMKE HAKI YA KUTOA MIMBA IWAPO NI MHANGA WA UBAKAJI?

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)*
Asiwe wangu wala wako; na akatwe. Ndipo mfalme akajibu, akasema, Mpe wa kwanza mtoto aliye hai, maana yeye ndiye mama yake. Na Israeli wote wakapata habari ya hukumu ile aliyoihukumu mfalme; maana waliona ya kuwa hekima ya MUNGU ilikuwa ndani yake, ili afanye hukumu" (1 Wafalme 3:16-28).

Ingekuwa jambo jema kwa wanawake wa leo wanaopenda kuua vitoto vichanga kuanza kuwa na moyo huo huo kama kahaba mwenye huruma aliyeelezwa hapo juu, ambaye alisema mwache mtoto! Alikuwa ni mama!

Mwigizaji Tony Curtis aliulizwa alikuwa ameonaje kumbusu Marilyn Monroe. Mrembo kama wanaume wengi walivyofikiri kuwa alikuwa, Tony Curtis alisema, "Ilikuwa kama kumbusu Hitler!" Nimesikia kwamba Marilyn Monroe ametoa mimba kadhaa, kwamba ameua vichanga kadhaa. Pengine hii ndiyo sababu Curtis, Myahudi, anazikumbuka kambi za kifo za Vita ya Pili ya Dunia, ambapo Wayahudi milioni sita wasio na hatia waliuawa na Hitler. Alidhani ilikuwa kama kumbusu Hitler alipoulizwa wakati alipombusu Marilyn Monroe katika filamu. Hivi ndivyo ninavyojisikia kuhusu wanawake wa leo wanaoamini katika utoaji wa mimba, uuaji! Mwanaume yeyote awezaje kutaka kubusu mmoja wao?

Zaburi 82:3-4 inasema, "Mfanyieni hukumu maskini na yatima; Mtendeeni haki aliyeonewa na fukara ["fukara" wakiwa ni wanadamu ambao hawajazaliwa ambao wanachukuliwa kama sio mwanadamu]. Mwokoeni maskini na mhitaji; Mwopoeni mikononi mwa wadhalimu." Fanya

*(Inaendelea ukurasa wa 8)*

## Kalifornia

Mchungaji Tony,

Nilitaka kukuambia kuhusu baba yangu. Baba yangu alinipigia simu leo na nilimuongoza kupitia sala ya mdhambi. Baba yangu alikuwa akilia machozi ya furaha na alisema alikuwa akisisimkwa mwili mzima na aliweza kuhisi Roho Mtakatifu. Alikuwa na furaha sana.

Nampa Mungu sifa sana na shukrani kwa uaminifu wake na ahadi zake, kwamba tukimtumikia kwa uaminifu, ataokoa nyumba yetu. Msifu Bwana.

Nilipojiunga na huduma, sikuwa na mawasiliano na baba yangu. Hakujihusisha na maisha yangu na sikuwa na wazo na alikokuwa au jinsi gani ya kuwasiliana naye ili niweze kumshuhudia. Nilimuuliza Bwana, "Namna gani nitamshuhudia baba yangu wakati sijui chochote kuhusu yeye au namna ya kuwasiliana naye?" Nilimwomba Bwana anifanyie njia.

Mungu aliniongoza. Babu yangu alinipa anuani ya baba yangu nami nikamwandikia baba yangu barua mwaka 2012. Takriban mwaka mzima ulipita na sikuwahi kupokea majibu. Nilijua kwamba baba yangu hakuwa na shughuli na mimi. Alimwacha mama yangu nilipokuwa na umri wa miaka tisa na kufanya uzinzi. Mimi na wazazi wangu tulikuzwa katika mafundisho ya uongo, tukiamini tumeokoka. Tuliamini "hakuna aliye mkamilifu" na "mara unapookoka, umeokoka daima"

Yapata miezi mitano iliyopita, baba yangu aliniita kanisani akisema alikuwa na barua niliyokuwa nimemwandikia. Nilimwambia baba yangu jinsi Bwana alivyoniokoa na nilikuwa nikimtumikia Bwana katika Huduma za Kikristo za Tony Alamo. Kwa miezi mitano iliyopita, nimekuwa nikimshuhudia Baba yangu, na nilimpelekea maandiko ya Injili.

Leo aliniita na alikuwa tayari kwa wokovu. Bwana Asifiwe! Ana furaha niko hapa nikiiwezesha huduma. Namshukuru Bwana kwa kumwokoa Baba yangu na kumrudisha maishani mwangu kwa sababu kwa zaidi ya miaka ishirini, hakuwepo. Asante, Yesu, kwa muujiza huu. Baba yangu anafahamu kuwa ameokoka sasa na anapaswa kushika amri za Mungu.

Praise the Lord!

Suzette Brown — Canyon Country, Kalifornia

## Zambia

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo,

Nawasalimu nyote katika jina la ajabu la Bwana wetu Yesu Kristo. Na awape Baraka tele nyote katika huduma yenu.

Nimepokea kifurushi ulichotuma. Asante. Majarida yako ya dunia yanawafanya watu wengi kuja kwa Yesu hapa. Yamenifanya hata niamue kusoma Theolojia. Tafadhali, ningependa kuwa msambazaji wako ili tuweze kumshindia Yesu roho nyingi.

Tafadhali nitumie Biblia na majarida mengine ili kazi ya Bwana isonge mbele.

Pole kwa habari mbaya niliyosoma kwenye barua yako, kwamba unateswa sana na serikali hapo. Daima naomba na kufunga kwa ajili yako ili Bwana Yesu Kristo aliyekufa kwa ajili ya kanisa awe nawe siku zote. Niliposoma kuhusu mateso yako, machozi yalitiririka usoni pangu. Ndugu, nakutia moyo ufanye kazi kwa bidii zaidi wakati unapoteswa. Hii inatuonyesha kwamba tunaishi katika dunia ambamo ibilisi yupo, lakini Wakristo si wa dunia hii. Inatubidi kufanya mapenzi ya Mungu, na si kile atakacho mwanadamu. Tutaendelea kukuombea hapa Zambia. Bwana atakuwa na watoto wake daima hadi mwisho tutakapomwona akija kutuchukua mawinguni. Amina.

Wako mtiifu,

Rick Makala — Chipata, Zambia

## Florida

Huduma za Tony Alamo:

Tumerudi kutoka kwenye ziara yetu na kijana wetu aliyejiunga na huduma miaka miwili iliyopita. Nilitaka kuwatumia ujumbe wale wasioamini. Hatukuwa waumini wa Huduma za Tony Alamo hadi kijana wetu alipojiunga, hata hivyo, hatukuwa na uhakika. Tumesoma mambo mengi mtandaoni kuhusu unyanyasaji wa watoto, vifungo vya jela, utumwa wa watoto. Kama ninavyoelewa, shutuma zilifanyika katika Arkansas. Hatukuona dalili zozote za mambo haya katika Kalifornia.

Zamani tulikuwa wakatoliki ambao wanamwamini Mungu lakini wasioamini mafundisho yote ya imani ya Katoliki.

Kijana wetu David alikuwa na matatizo mengi ambayo hatuwezi kueleza. Alipatwa na tatizo la kiafya la mfadhaiko/huzuni alipokuwa katika miaka ya utotoni. Tulijaribu mambo mengi kutuliza hili – dawa, ushauri nasaha, mlo, na mazoezi. Hakuna kilichosaidia. Miaka ilivyoendelea, alizama zaidi kwenye mfadhaiko, na uzito wake ukaongezeka ghafla. Hatukuwa tukienda kanisani mara kwa mara na hata nilipomtaka David kuungana nasi kanisani, hakuwa na nia.

Leo angekwambia kwamba haamini uwepo wa Mungu. Alijihusisha na Mitandao ya Intaneti na jambo moja likaanzisha lingine. Aliondoka nyumbani kwetu na akapata faraja kwa bibi yake huko Michigan. Alipofariki bibi yake, David aliona njia ya kwenda kwa Huduma ya Kikristo ya Tony Alamo, shukrani kwa Gail Brubach ambaye alikuwa mtu muhimu kumleta David Kanisani.

Tulimwombea David kila siku ili awe na furaha. Tulijua kidogo kuwa Mungu alikuwa akishughulika nalo, Mungu huyu ambaye David hakumjua awali. Dakika tuliyopiga hatua kuingia kwenye kanisa la Huduma za Kikristo za Tony Alamo tulimwona kijana wetu. Tuliweza kuona tangu alipowasili, kulikuwa na tofauti kubwa ambayo ni njema. Uzito wake ulikuwa umepungua, huzuni yake ilikuwa imetoweka (niliona mara moja tabasamu usoni pake na mwanga mpya aliokuwa amepata), na mtazamo wake wa maisha ulikuwa umebadilika kabisa. Alikuwa sasa akimfanyia kazi Mungu.

Sikuwa muumini wa Huduma hii ya Kikristo (si wa Mungu), lakini niliweza kuona nguvu ambazo Mungu alikuwa nazo juu ya mtoto (sasa ana miaka 31, si mtoto tena) ambaye awali alikuwa si mtu wa kanisa kwa namna yoyote, hakuiamini Biblia, na alikuwa mpinga-kanisa katika kila njia. Tulipokuwa tukihudhuria huduma za kanisa, tulianza kuelewa nguvu ambazo Biblia ilimtia kila mtu. Kweli tunasoma Biblia, na kuimba nyimbo ambazo zilifungua mioyo yetu. Zilikuwa ni siku nne za kuwa kanisani kwa hiari ambazo tumewahi kuwa nazo.

Usiku wa kwanza, nyimbo zilikuwa za kusisimua sana, na huduma ilikuwa ikisonga, shukrani tena kwa Gail Brubach, nilikuwa nimeokoka. Machozi yalikuwa yakitiririka usoni mwangu. Sijawahi kupata uzoefu wa huduma ya kanisa iliyogusa jinsi ile. Usiku wa siku tatu zilizofuata tulizoweza kuwa pale zilikuwa zikigusa jinsi ile ile, na tulihuzunika ilipotubidi kuondoka. Tumekutana na baadhi ya washiriki wa kanisa wa ajabu.

Huduma za Kikristo za Tony Alamo zinafungua milango kila usiku kwa watu wengi wasio na makazi. Katika Los Angeles, bure bila malipo, wanasafirishwa kanisani ambapo huduma nzuri zinaendeshwa na muziki wa kusisimua. Baada ya huduma, mlo kamili unatolewa bila malipo kwa wanaohitaji. Sijawahi kuona unyanyasaji wowote, ila upendo tu kwa wapendwa waume/wake. Kanisa hili ni nyota ing'arayo. Mungu amewaweka hapa kwa kusudi. Kama ilivyo katika kifungu cha Biblia kitabu cha Mathayo 20:27-34:

"Na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu, na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengine. Hata walipokuwa wakitoka Yeriko mkutano mkubwa wakamfuata.

Na tazama, vipofu wawili wameketi kando ya njia, nao waliposikia ya kwamba Yesu anapita, walipaza sauti, wakisema, uturehemu, Bwana, Mwana wa Daudi! Yesu akasimama, akawaita, akasema, mnataka niwafanyie nini? Wakamwambia, Bwana, twataka macho yetu yafumbuliwe, Yesu akawahurumia, akawagusa macho yao; mara wakapata kuona, wakamfuata."

Kimsingi, ujumbe wangu ni – unapokuwa umeguswa na Mungu, macho yako yatafunguka, kama yetu yalivyofunguliwa kanisani. Ulikuwa ni uzoefu usio wa kawaida. Natumaini wengine wataliona kanisa. Mara macho yako yatakapofunguliwa kama yetu, utaweza kuona pia.

Wako waaminifu,
Sherry and David M. Palmisano
North Port, Florida

## Mexico

*(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)*

Natumaini hujambo, ukiwa umezungukwa na watu wa imani. Nataka kuwashukuru kwa mawasiliano yote ambayo mnasumbuka kunitumia, kwa maandiko yote mnayonitumia, ambayo yananifanya niakisi na kuendelea na imani yangu thabiti ya kutaka kurekebisha njia yangu na kumshukuru Mungu Baba kwa Baraka zake zote. Natumaini mtaendelea kuwahamasisha waumini wote kubadilika na kuendelea katika njia za kweli. Ni matumaini yangu, katika jina la Bwana Yesu, Mungu anawaruhusu kuendelea na kazi hiyo kubwa mno na kanisa lenu litaendelea mbele kama mnara wa taa katikati ya tufani.

Nakutakia kila la heri kutoka kwangu. Mungu akutunze na kukulinda na aendelee kukuongoza. Usikome kutuweka sisi wafungwa katika sala zako, na kama ukiweza, tutumie Biblia ili tusiwe fukara. Sina la ziada kwa sasa.

Mungu akutunze kwa muda mrefu na kwa wema.

Jose Martin Cortes Murillo
Durango, Mexico

## Pennsylvania

Mchungaji alipiga simu kutoka Pennsylvania kusema alijifunza kwa mara ya kwanza kuhusu kanisa mwaka 1973, na kwamba amekuwa akitumia maandiko ya Mchungaji Alamo kufikisha ujumbe kwa mkutano wake. Alisema maandiko ya Mchungaji Alamo yanajieleza kwa kina kiasi ambacho anaweza kupata ujumbe 30 kutoka kwenye kipande kimoja cha maandiko. Aliomba nakala 25 za majarida ya hivi karibuni ili apate jumbe zaidi wa kuufikishia mkutano wake.

# Ushuhuda wa Sally Demoulin


*Dada Sally Demoulin*

Kwanza kabisa, nataka kuanza kwa kushukuru na kumsifu Bwana Yesu Kristo kwa kumwaga damu yake ya thamani na kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu na dhambi ya ulimwengu; zawadi ya mwisho kwa ajili yetu kuwa na uzima wa kweli na wa milele katika Ufalme wa Mbinguni.

Bwana alikutana nami miaka 28 na nusu iliyopita. Sikuwa nikimtafuta Mungu, wala sikujua kwamba nilikuwa nimepotea. Nilizaliwa katika Brooklyn, New York, na kukulia kwenye Ukatoliki. Ninakumbuka kati ya umri wa miaka 15 au 16 nilipokuwa kwenye boti ya kivuko kwenye mto Hudson, nikiwa nikitalii huku na kule. Kisha tukapita jabali lililokuwa na maandishi "Yesu anaokoa" yameandikwa kwa herufi kubwa nyeupe. Mawazo yangu ya kwanza yalikuwa "Anaokoa? Anaokoa kutoka kwenye nini?" Nikiwa nimekulia kwenye Ukatoliki, sikuwahi kusikia kuhusu wokovu, wala Yesu aliyeokoa.

Wazazi wangu walikuwa wakali sana kwangu, hivyo katika umri wa miaka 18, niliamua kwamba nilikuwa mkubwa vya kutosha kufanya nilichotaka kufanya bila ya wao kuniambia nini ninachoweza kufanya au nisichoweza kufanya. Niliondoka nyumbani mwa wazazi wangu ili niweze kuwa "huru," au hivyo nilivyowaza. Miezi kadhaa baadaye, nilijikuta nimeolewa; mwaka mmoja baadaye nilikuwa na mtoto. Mara tu nilipodhani maisha yalikuwa mazuri nikidhani nina furaha, mambo yakawa machungu; na miaka kadhaa baadaye nilitalikiwa, mama bachela. Hivyo hapa nikawa "huru" tena na nilikuwa nikitaka jambo hilo libaki hivyo kwa sababu sikutaka kumwegemea au kumtegemea mtu yeyote. Nilikuwa na akili ya namna hiyo kwamba naweza kufanya mambo vizuri mimi binafsi.

Nilikuwa na kazi nzuri inayolipa, nyumba nzuri na sikupungukiwa chochote. Nilihakikisha kuwa mtoto wangu na mimi tulikuwa na chochote tulichohitaji na kukitaka. Nilikwenda tu kwenye biashara zangu na niliishi maisha kama ilivyonipendeza. Wakati mwingine baadaye nilijikuta kwenye uhusiano mwingine. Miaka michache baadaye, niligundua kwamba mwanamume huyu alikuwa akijihusisha na heroin na alikuwa akiiba na kudanganya ili kupata fedha alizokuwa akihitaji kwa ajili ya tabia yake ya madawa. Nilificha hisia zangu zote na matatizo ndani yangu. Kwa watu waliokuwa wananijua, ilionekana kama vile nilikuwa naendelea vizuri sana na mwenye furaha. Lakini nilikuwa mwenye huzuni sana, asiye na furaha na kutaka mabadiliko lakini sikujua la kufanya. Mambo yalikuwa mabaya sana kiasi cha kwamba nilitaka kuondoa uhai wangu. Nilifikiria kumeza vidonge vilivyojaa chupa na kufa tu. Lakini niliogopa kile kingetokea baada ya mauti na kile kingempata mtoto wangu baada ya mimi kufa. Nilikaa chini, nikalia na kumuuliza Mungu kuyabadili maisha yangu.

Baada ya muda, nilidhani kuwa labda yote niliyotaka kufanya ni kubadili namna nilivyofikiri, hivyo nilianza kusoma vitabu mbalimbali vya kujisaidia-binafsi ambavyo vilikuwa sokoni: "Mtazamo Chanya," "Dayanetiki," "Imani ndiyo Jibu," chochote kinachohusika na mada hizi nilisoma. Lakini jinsi nilivyosoma vitabu vingi zaidi, ndivyo nilivyozidi kuchanganyikiwa. Kulipokuwa hakuna mabadiliko, niliamua kwamba nilihitaji kurudi kanisani. Hivyo muda wa chakula cha mchana, nilikwenda Kanisa la Kidayosisi la Mt. Patrick katika Jiji la New York, ambalo lilikuwa karibu na kazini kwangu, na niliingia ndani, nikawasha mshumaa na kupiga magoti chini na kusali. Lakini nilitoka nje nikiwa najisikia vibaya mno kuliko nilipoingia ndani. Siku moja nakumbuka nilikwenda kwenye jengo la "kanisa" hilo, nikijisikia kufadhaishwa sana. Niliketi na kutazama jengo lile kubwa nikagundua kwamba juu ya nguzo kulikuwa na mizalimu yenye sura mbaya, kitu ambacho nakumbuka nikikiona kwenye filamu ya *The Omen*. Nilipigwa na butwaa na nikaanza kutafakari binafsi "kitu kibaya mno duniani kilikuwa kinafanya nini katika sehemu ambayo ilikuwa inastahili kuwa takatifu?" Nilitoka nje na nikavuka mtaa ili kutazama vyema nje ya jengo kutokea mbali na nikatambua kwamba aina ile ile ya viumbe wabaya ilikuwa kwenye pembe za jengo. Bila kuwa na haja ya kusema, sikuweka mguu wangu ndani ya jengo lile au jengo lolote la Katoliki baada ya hapo.

Basi Jumamosi moja mnamo Februari ya 1985, nilikwenda kufanya manunuzi na mwanangu. Siku hiyo ilikuwa na joto lisilo la kawaida. Ilipaswa kuwa baridi ya kugandisha, lakini jotoridi lilikuwa lapata nyuzi joto 75, iliniogopesha. Nilihisi kama kitu fulani hakikuwa sahihi kabisa na dunia ilikuwa inaelekea mwisho. Sikuwa najua jambo hili wakati ule, lakini najua sasa kwamba alikuwa ni Roho wa Bwana aliyenifanya nijue jambo hili. Nilipata hofu.

Majuma mawili baadaye, nilishuhudiwa na ndugu wawili kutoka taasisi ya Kikristo ya Tony na Susan Alamo, ambao walikuwa mahali katika Brooklyn wakitafuta roho zilizopotea. Niliambiwa ni kwa nini Yesu alimwaga damu Yake na kufa msalabani; kwamba kulikuwa na Mbinguni na Kuzimu; na kwamba kama ningekufa na dhambi rohoni mwangu ningekwenda kuzimu milele, na hakungekuwa kutoroka. Kwa kiburi changu, nilikuwa nimesahau kabisa hofu niliyopata majuma mawili kabla. Sikudhani kwamba nilimuhitaji Yesu au Mungu. Lakini namshukuru Mungu kwa kuwa hakuchoka kushughulika na mimi. Majuma machache baadaye, nilijikuta nikiongea kwenye simu na mtu mmoja kutoka kanisani nikisema ile sala ya kizamani iliyopitwa na wakati ya mdhambi ya kutubu na kumkubali Bwana Yesu Kristo moyoni mwangu. Mara nilipomaliza kusema sala ile, nilijisikia mwepesi kama unyoya. Dhambi zangu zilikuwa zimeoshwa zote katika damu ya thamani ya Yesu. Nikawa mzima, Nilijihisi kuwa mpya. Nilikuwa na furaha ambayo siwezi kuielezea

kwa maneno. Nilihisi kuwa hai kweli kwa mara ya kwanza maishani mwangu, na nilikuwa na amani.

Nilianza kwenda kwenye kanisa letu lililokuwa mbele ya duka kule Brooklyn. Tulikuwa na huduma, chakula baadaye na kisha tukawa na vikundi vya kusoma Biblia. Nilikwenda kila usiku; nilitaka kujua zaidi kuhusu maisha mapya ya ajabu niliyokuwa nayo katika Kristo. Ndugu wale wawili walinihamasisha kuhamia kwenye huduma ili niweze kuwa karibu na dada wengine wa Kikristo na familia, na kukua imara katika Bwana. Waliniambia kuhusu uwezeshwaji mzuri katika Arkansas ambao ulikuwa wa kurahisisha maisha ya familia; waliongea kuhusu mikutano ya maombi ambayo ilitendeka mara mbili kwa siku, shule ya Kikristo yenye mtaala wa Kikristo, bwawa lenye ukubwa wa ki-Olimpiki na maeneo ya kucheza kwa ajili ya watoto. Na vyote vilikuwa vyema, lakini sikutaka kwenda mbali na mazingira niliyokuwa nimezoea. Nilitaka niweze kubaki Brooklyn na kwenda kanisani tu. Vyema, Bwana alikuwa na mipango mingine kwa ajili yangu. Ilikuwa inakwenda kuwa njia yake.

Mwishoni mwa juma siku ya kumbukumbu mwaka huo huo, tulikuwa katika bustani ya Coney tukisambaza maandiko ya Injili na kuzishuhudia roho. Nilitaka kwenda msalani na kulikuwa tu na mahali pamoja pa kwenda ambapo ilinibidi kupitia upande mwingine wa baa. Nilitembea kupitia kwenye baa kwenda kwenye eneo la msala, na kwa sababu kulikuwa na tatizo la msala, ilinibidi kusubiri kwenye foleni. Nilipokuwa nikisubiri, nilitazama watu waliokuwa wakinywa vileo katika baa tulivu, wakicheza na kuendelea, nikifikiri kuwa walikuwa na wakati mzuri. Ghafla, Bwana akanipa maono ya wazi; kila kitu kiligeuka giza, na kulikuwa na miale ya moto, na watu wale waliokuwa wakicheza walionekana kama vivuli vyeusi vilivyokuwa vikigongana. Ilikuwa kama vile naitazama kuzimu kutokea nje, lakini niliweza kuhisi joto kutoka kwenye miale ya moto. Ilidumu kwa muda mchache tu, lakini nilihisi kama milele. Ilipokwisha, hakuna maneno yanayoweza kuelezea hofu niliyopata, na Bwana akanipa ufahamu kwamba niondoke kutoka pale na kuhamia kwenye huduma. Sikuweza kutoka nje ya Brooklyn kwa haraka vya kutosha. Mipango ilifanyika, na tulihamia kwenye huduma muda mfupi baada ya kutoa notisi kwa mwajiri wangu. Nimekuwa katika Huduma za Kikristo za Alamo tangia hapo.

Nilipohamia kwenye Huduma za Kikristo za Alamo, Niligundua kwamba tunalo kanisa katika Los Angeles, CA, ambapo kwa mara ya kwanza huduma ilianzia na ambapo mia elfu nyingi za roho zimeongolewa na Bwana. Ilikuwa inasisimua sana pia kusikia kuhusu makanisa kote duniani ambayo yalikuwa matokeo ya watu waliotoa maisha yao kwa Bwana baada ya kusoma ujumbe Mungu aliompa Mchungaji Alamo naye akausambaza kwa Ulimwengu.

Huu ni mwanzo tu wa hadithi yangu. Yapo mengi sana ambayo Mungu ametenda katika kipindi hiki cha miaka 28 na nusu. Miaka mizuri katika maisha yangu. Siwezi kuibadilisha kwa kitu chochote ambacho dunia inaweza kutoa, kwa sababu kila kitu itoacho dunia hutuongoza kwenye kifo na Jehannamu, lakini kila kitu atoacho Mungu kinatuongoza kwenye uzima, uzima tele, na kisha umilele Mbinguni. Bwana Yesu Asifiwe!!!!
Sally Demoulin

## Nigeria

Tony Alamo, Mchungaji wa Dunia,

Nimepitia maandiko yote ya Injili, vitabu, CD ulizonitumia na nimegundua kwamba nina maono sawa na wewe na nimeamua kuwa kundi moja nawe, kwa hali yoyote ile.

Nimemuoa Mwinjilisti (Bi.) Betty Igba tangu 1988. Tumebarikiwa kuwa na watoto wawili – Naomi na Joshua. Tunalihubiri Neno la Mungu kwa waliopotea tangu miaka 13 iliyopita. Nitafurahi sana kama unaweza kunifikiria na kuniteua mimi kama mmoja wa wachungaji wako katika Afrika kwenye huduma yako, Kanisa la Kikristo la Tony Alamo. Nimeanza kukusanya na kufundisha mashujaa wa maombi kwa ajili ya maono haya. Natarajia wafuasi milioni moja kwa ajili ya Kanisa la Kikristo la Toni Alamo, Owerri, Nigeria.

Mungu na awajaze nyote hapo mnapoendelea kuufanya mwanga wa huduma uangaze. Msikate tamaa kwa sababu kilio kitadumu usiku, bali furaha yaja asubuhi. Muujiza wenu upo njiani.



*Mch. Eleazer Igba (mwenye kipaza sauti) akileta Injili katika shule za Owerri, Jimbo la Imo, Nigeria, kwa Maandiko ya Mchungaji Alamo yaliyojazwa kwa roho.*

Mimi na mke wangu, Betty, tumekuwa tukifanya uinjilisti ndani na nje ya jiji letu kwa maandiko ya Kikristo ya Tony Alamo, na roho nyingi zinakuja kwa Kristo kwa kasi ya Mungu. Hata Wakatoliki na wafuasi wa wachawi wanatubu kwa kasi sana baada ya kusoma maandiko.

Mungu Mwenyezi aliyewainua juu asiwaangushe, Amina. Mama Easther Igba anasema wewe ni wa ajabu.

Wako mtiifu,
Mch. Eleazer Igba
Igba Owerri, Jimbo la Imo, Nigeria

# JE! MUNGU ANAMPA MWANAMKE HAKI YA KUTOA MIMBA IWAPO NI MHANGA WA UBAKAJI?

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 4)*

hivi uishi (milele). Tubu dhambi zako zote. Sali sala hii:

**BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi[4] ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.[5] Ninaamini kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.[6] Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU[7] na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.[8] Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.[9] Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,[10] hutanikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia, linasema hivyo.[11] NENO LAKO linasema hutamkataa yeyote na mimi nikiwemo.[12] Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.[13] Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonyesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.[14]**

Sasa kwa kuwa umeokoka, mtumikie MUNGU kwa moyo wako wote, roho yako yote, akili zako zote na kwa nguvu zako zote (Marko 12:30).[15] Ubatizwe kwa kuzamishwa kwenye maji, kwa jina la BABA, la MWANA, na la ROHO MTAKATIFU.[16] Kwa bidii soma Biblia Takatifu (toleo la The Bible League – Waenezaji wa Neno la MuNGU TANGU 1938) na ufanye kile isemacho mpaka siku utakayokufa.[17]

Basi, kama YESU alivyoamuru, umshindie roho. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwa msambazaji wa Maandiko ya Mchungaji Alamo. Tunachapisha maandiko ya Mchungaji Alamo katika lugha nyingi, na tunayapeleka ulimwenguni kote. Tunatumia mamilioni ya dola kununua karatasi na usafirishaji, hivyo tunahitaji maombi yenu na msaada wa kifedha.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:8-12).

---

**4** Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 **5** Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 **6** Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 **7** Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 **8** Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 **9** 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 **10** Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 **11** Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 **12** Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 **13** Ebr. 11:6 **14** Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 **15** Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 **16** Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18 **17** Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

*Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:*

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**

**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**

**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

*Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa mioyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.*

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**

**Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

*Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo*

*Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.*

*Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.*

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)**

**USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**

© Hatimiliki Desemba 2013, 2015 Haki zote zimehifadhiwa Mchungaji wa Ulimwengu Tony Alamo ® Imesajiliwa Desemba 2013, 2015

SWAHILI—VOLUME 18700—*DOES GOD PERMIT A WOMAN THE RIGHT TO HAVE AN ABORTION IF SHE IS A VICTIM OF RAPE?*